Australian Government
Department of Education and Training

Mpango wa Kiingereza cha Mtu Mzima Mhamiaji (Adult Migrant English Program)

Kiingereza ni lugha ya taifa ya Australia. Watu nchini Australia husemaa lugha nyingi, lakini kusema na kuelewa Kiingereza itakusaidia kushiriki kikamilifu katika maisha ya Australia. Bila Kiingereza, utaona ni vigumu kupata Uraia wa Australia, kupata huduma muhimu na kujitegemea.

Kukusaidia kujifunza Kiingereza, unaweza kujiunga Adult Migrant English Program (AMEP).

AMEP ni nini?

AMEP inafadhiliwa na Serikali ya Australia (Australian Government) na hutoa hadi masaa 510 ya masomo ya lugha ya Kiingereza bila malipo kwa wahamiaji wanaostahili na waingiaji waliohurumiwa. Kama umepewa visa ya kudumu au visa ya muda mfupi yenye kustahili na unasema Kiingereza kidogo au hujui, unaweza kustahili AMEP. Vijana wahamiaji wengine wenye umri kati ya miaka 15 na 17 wanaweza pia kustahili.

Katika darasa la AMEP, utajifunza ustadi wa lugha ya Kiingereza na habari kuhusu jumuiya ya Australia. Utakutana na wanaowasili wengine wapya na kupata marafiki wapya. Hizi pamoja itakusaidia wewe na familia yako kuishi kwa ufanisi nchini Australia. Ustadi wa lugha ya Kiingereza pia ni muhimu sana kama ukitaka kufanya kazi nchini Australia

AMEP hutolewa na watoaji huduma waliokubaliwa na hufundishwa na walimu ambao wamefunzwa kufundisha Kiingereza kwa wasemaji wa lugha nyingine.

Nawezaje kujiandikisha?

Kupata masomo ya lugha ya Kiingereza kupitia AMEP, unapaswa kujiandikisha watoaji wa huduma wa AMEP waliokubaliwa ndani ya muda wa miezi sita ya kuwasili nchini Australia au kutoka mwanzo wa visa. Unapaswa kuanza masomo ya Kiingereza ndani ya miezi 12 ya kuwasili nchini Australia au kutoka mwanzo wa visa yako.

Una muda wa miaka mitano kuanzia tarehe yako ya kuwasili nchini Australia au siku ya visa kuanza ili kujifunza Kiingereza kupitia AMEP. Unaweza kustahiki masomo ya ziada kulingana na mahitaji yako.

Mtoaji huduma wako atakusaidia kuchagua darasa ambalo litafaa sana kwa mahitaji yako ili kuhakikisha itakupa matokeo bora kwako iwezekanavyo . Kuna masomo ya muda wote na ya muda maalamu kwa nyakati tofauti na katika maeneo tofauti hivyo unaweza kujifunza wakati na mahali panapofaa kwako.

Mikondo ya mafunzo

Ili ndipo uweze kulingana mahitaji yako, mtoaji huduma wako wa AMEP atakusaidia kuchagua kutoka kwa mikondo miwili ya mafunzo:

- Mkondo wa Kiingereza wa kabla-ajira – kwa wateja wanaotaka kutegemea Kiingereza ili kushiriki katika mahali pa kazi, au mafunzo ya ziada yanayoweza kuchangia kupata ajira endelevu.
- Mkondo wa Kiingereza cha Jamii - kwa wateja wanaotaka kuboresha uwezo wao katika kuongea Kiingereza ili kuwasaidia kushiriki kwa kijamii na kupata ujasiri wa kuishi kwa kujitegemea ndani ya jamiii yao.

Unaweza kutumia ustahiki wako wa kisheria wa masaa ya 510 katika ama mkondo au kwa mchanganyiko wowote.

Wateja wanaopokea msaada wa malipo ya mapato wenye mahitaji ya wajibu wa pande mbili hawatastahiki kupata mkondo wa Kiingereza ya Jamii.

Je, kama siwezi kwenda darasani?

Kama huwezi kuhudhuria masomo yako, zungumza na mtoaji huduma wako wa AMEP. Mtoa huduma huyo huenda anaweza kukusaidia kujifunza Kiingereza na mwalimu wa nyumbani au mtandaoni na mafunzo ya mtandaoni ya AMEP kupata msaada kutoka kwa mwalimu.

Unaweza pia kujifunza kwa kasi yako mwenyewe kwa kutumia modyuli za kibinafsi za kujifunza za AMEP zinazopatikana kwa www.amepdl.net.au. Masomo haya ya bure yanapatikana kwa kila mtu (si tu kwa wateja wa AMEP) kuwasaidia watu kujifunza Kiingereza.

Mipango midogo ya AMEP

Unaweza kustahiki mafunzo ya ziada kama una mahitaji maalum.

Mpango Maalum wa Maandalizi (Special Preparatory Program)

Special Preparatory Program (SPP) inatoa masaa ya ziada na msaada kwa washiriki na waingiaji wanaostahiki walio na matatizo ya kabla-kuhama na kupata nafasi chache ya mafunzo.

Njia za Lugha ya Kuzoea kwa Ajira na Mafunzo (Settlement Language Pathways to Employment and Training)

Mpango wa Settlement Language Pathways to Employment and Training (SLPET) huwapa wanafunzi wanaostahiki kozi inayolenga ajira ili kuwasaidia kujifunza Kiingereza cha shughuli maalum wakati wanapoanza kuzoea utamaduni na utaratibu wa mahali pa kazini nchini Australia.

SLPET hutoa hadi masaa 200 ya ziada ya mafunzo ya Kiingereza cha shughuli maalum, ikiwa ni pamoja na hadi masaa 80 ya nafasi ya uzoefu wa kazi katika viwanda mbalimbali tofauti.

Nyongeza ya AMEP (AMEP Extend)

Mpango wa AMEP Extend hutoa hadi masaa 490 ya masomo ya ziada kwa wanafunzi wanaostahiki ambao wanakamilisha masaa 510 yao bila kutimiza malengo yao ya ustadi wa lugha ya Kiingereza.

Matunzo ya Mtoto ya AMEP (AMEP child care)

Mtoaji huduma wako wa AMEP anaweza kupanga matunzo bure ya watoto wakati unapohudhuria masomo. Matunzo ya bure ya mtoto hutolewa tu kwa watoto walio na umri wa chini ya kwenda shuleni.

Ushauri wa njia wa AMEP (AMEP pathway guidance)

Watoaji huduma wa AMEP hutoa ushauri wa njia ili kukusaidia kuweka malengo, kuelewa chaguzi zako na kufanya maamuzi kuhusiana na masomo yako, kuendeleza masomo na nafasi za ajira.

Kwa habari zaidi

AMEP	Habari za mawasiliano
Simu	13 38 73
Tovuti ya AMEP	www.education.gov.au/amep
Barua pepe	skilling@education.gov.au
Habari katika lugha tofauti na Kiingereza	www.education.gov.au/amep-information-other-languages
Wapi naweza kujifunza Kiingereza?	www.education.gov.au/adult-migrant-english-program-service-providers
AMEP mtandaoni	www.amepdl.net.au